THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education

**102/2** **Karatasi ya 2**

# KISWAHILI

## LUGHA

**Dec. 2022 – Muda: Saa 2½**

---

**Jina** .................................................................................. **Nambari ya Mtahiniwa** ....................................

**Sahihi ya Mtahiniwa** ...................................................... **Tarehe** ............................................

---

421

**Maagizo**

(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali **yote**.
(d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
(e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
(g) **Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa**.
(h) **Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo**.

0466

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

© 2022 The Kenya National Examinations Council


317136

## 1. UFAHAMU (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Ziara ya wanafunzi wa Chama cha Mazingira kutoka shule ya Faidi ilikuwa ya kuvutia. Mara tu walipofika kwenye lango la uwanja wa maonyesho, walikaribishwa kwa ngoma za kitamaduni. Vilevile, vikundi tofauti vya muziki vilipishana kuwalaki wageni kwa miondoko yao.

"Haya, mmejionea, mwacha mila ni mtumwa," alisema mwalimu Mkala akiwaelekeza wanafunzi wake kwenye sehemu nyingine za maonyesho. Huko ndani walijionea mengi. Waliona vielelezo na kupewa maelezo kuhusu mbinu mpya za kilimo. Mbinu hizo zilikuwa na azma moja; kuhifadhi mazingira. Uhifadhi wa maji, miti na wanyamapori ni baadhi ya mambo yaliyotiliwa mkazo. Wanafunzi nao walibaini kuwa viumbe hutangamana na kutegemeana. Lena, mwenyekiti wa Chama cha Mazingira alivutiwa na sehemu ya maonyesho iliyohusu mbinu za kisasa za ufugaji. Alistaajabishwa na maelezo kuhusu ufugaji wa wadudu.

"Lo! Wanafuga konokono; tena wanaliwa?" Lena alimuuliza mwalimu wake kwa sauti ya chini.

"Naam, wadudu wanaofugwa na wanaoliwa ni wengi. Huu ni mwanzo tu, hatujafikia kwenye kibanda cha kumbikumbi na chenene. Waandalizi wa maonyesho haya walitangaza kuwa kibanda hicho kitakuwepo." Mwalimu alimjibu Lena.

Baada ya kukamilisha ziara yao, wanafunzi walikuwa wameshiba kwa mafunzo na maelezo mapya ya namna ya kuhifadhi mazingira na kuzalisha chakula.

"Natumai mmejifunza mengi ambayo yatawafaa na kuwafaidi wengine. Utamu wa elimu ni kuelimishana. Najua mtaipanda mbegu ya maarifa mliyopewa leo istawi na kuzaa matunda." Mwalimu Mkala aliwaambia wanafunzi wake.

Basi lao liliposhika baraste kuu, Lena alizama kwenye mawazo. Mara wazo lilimjia. Aliona kwamba kuna uwezekano wa kikundi cha Wanarika katika kijiji chao kuanzisha mradi wa kufuga wadudu.

"Sofi, unaonaje tukianzisha mradi wa kufuga vipepeo kijijini mwetu wakati wa likizo?" Lena alimuuliza rafiki yake.

"Lena, mradi wa vipepeo unahitaji kundi kubwa la watu ili ufanikiwe. Utahitaji ushirikiano wa wanakijiji wote. Je, utaweza?" Sofi alimuuliza Lena.

"Utaweza Lena, Sofi asikuvunje moyo. Unachohitaji ni nia na ari ya kutimiza maono yako." Mwalimu Mkala alimhimiza Lena.

Ushauri wa Mwalimu Mkala ulimpa Lena mshawasha wa kuanzisha mradi huo. Wakati wa likizo, Lena aliwaarifu baadhi vijana katika kijiji chao kuhusu wazo lake. Pendekezo hili lilipokelewa kwa hisia tofauti. Waliovutiwa walikuwa wengi. Walilikumbatia pendekezo hilo likawa si wazo la Lena tena bali lao.

Papo hapo, vijana walianza **mchakato** wa kuhakikisha mradi wao umefaulu. Lena alimwalika Chifu wa eneo lao katika mojawapo ya mikutano yao. Chifu aliwaelekeza kuhusu namna ya kupata leseni. Kisha, akawatengea sehemu ya uwanja wa umma palipo na bustani ili kufanyia shughuli zao. Kwenye bustani mlikuwa na vipepeo wachache. Vijana waliimarisha mazingira ya pale kwa kupanda miti ya kiasili na bustani za maua ili kuwavutia vipepeo zaidi. Vipepeo walizaana. Kukawa na vipepeo wa rangi anuwai na maumbile mbalimbali. Vijana walisakura kwenye mtandao na kupata maarifa zaidi kuhusu maisha ya vipepeo na namna ya kuwatunza.

Polepole, mradi wao ulianza kuzaa matunda. Picha na video za vipepeo wa kupendeza walizoweka kwenye mitandao ya kijamii ziliwavutia wengi. Aidha, Lena na viongozi wenzake walialikwa kwenye kituo maarufu cha runinga kuelezea zaidi kuhusu mradi wao.



Teacher.co.ke

"Je, mradi wenu unawafaidi vipi?" Mwanahabari aliwauliza akina Lena.

"Mradi wetu una faida kochokocho. Kwa mfano, mazao shambani yameimarika kutokana na vipepeo kusambaza mbegu kwenye maua ya mimea. Nyuki pia wameongezeka. Watu wametundika mizinga kwenye miti ya kiasili na wengine tayari wanarina asali. Faida ni nyingi ila hazionekani kwa macho," alieleza Lena huku akitabasamu. Wenzake pia walitoa michango yao.

Habari ya kijiji chao zilienea kwa **kasi ya moto wa nyikani**. Kijiji kikapata jina jipya – Kijiji cha Vipepeo. Isitoshe, Lena na wenzake walipata ufadhili wa kuendeleza masomo yanayohusiana na mradi wao na suala zima la mazingira. Vilevile, walipokea mialiko ya kitaifa na ya kimataifa ili kuzungumzia mradi wao.

Kijiji chao nacho kilifaidi si haba. Viongozi walishikana na kujenga kituo kikubwa cha kulea na kutafitia vipepeo. Watalii waliozuru kijiji chao ili kujionea vipepeo na kuwafanyia utafiti walitozwa ada. Ada hii ilidunduizwa na kuwekwa katika hazina ya kuendeleza miradi ya kijiji chao. Sura ya kijiji ilibadilika, barabara, hospitali na shule zikajengwa na zilizokuwepo zikaimarishwa.

(a) Eleza jinsi Mwalimu Mkala alivyowafaa wanafunzi kwa mujibu wa kifungu. (alama 2)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

(b) "Wanafunzi nao walibaini kuwa viumbe hutangamana na kutegemeana." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hoja **tano** kutoka kwenye kifungu. (alama 5)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

Teacher.co.ke

(c) Wanachama wa Chama cha Mazingira walipanda mbegu ya maarifa, ikastawi na kuzaa matunda. Fafanua kauli hii kwa mujibu wa kifungu. (alama 3)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(d) Andika **mambo mawili** yanayoonyesha kuwa Lena ni mkakamavu. (alama 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(e) Eleza maana ya: (alama 2)

(i) mchakato ..........................................................

(ii) kasi ya moto wa nyikani ................................

(f) Kipe kifungu hiki anwani mwafaka. (alama 1)

..........................................................................................................................................

Teacher.co.ke

421

0466

## 2. UFUPISHO (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Vijana wanapomaliza kozi fulani, matarajio yao ni kupata ajira. Kati ya vijana wanaohitimu katika vyuo, shule za sekondari na za msingi ni wachache sana wanaopata ajira. Hili linatokana na tatizo kuu la ukofesu wa ajira nchini Kenya na ulimwenguni kwa jumla. Ikumbukwe kwamba kati ya watu kumi humu nchini, saba ni vijana walio chini ya miaka thelathini na mitano. Hii ina maana kwamba nafasi za ajira ni chache ikilinganishwa na idadi ya vijana.

Japo serikali imewekeza katika maswala ya vijana, ajira kwa vijana ingali tatizo linalohitaji suluhisho la kudumu. Tafiti zinaonyesha kwamba uhaba wa ajira husababishwa na mambo anuwai. Ilivyo sasa ni kuwa, maarifa aliyo nayo mtu ndiyo huchangia katika kuajiriwa kwake. Hata hivyo, wapo wale ambao hawapati ujuzi na maarifa ya kutosha kwa sababu ya kukosa makini wakati wa mafunzo. Vilevile, inawawia vijana vigumu kupata ajira ama kwa kuwa hawakukamilisha kozi fulani au hawakupata ujuzi wa kuwawezesha kuajiriwa. Si ajabu kupata vijana ambao wanapata ajira ila wanakosa kuwajibika na hivyo kuachishwa kazi. Hawa utapata wanachelewa kufika kazini, wanakosa kukamilisha kazi walizopangiwa, wanakosa kufika kazini bila idhini, na hata kukosa kushirikiana na wenzao.

Isitoshe, baadhi ya vijana wana mazoea ya kuchagua kazi na kudharau kazi nyingine. Wao hupendelea kazi za ofisini na kupuuza zile zinazodhaniwa kuwa za sulubu. Ukiwauliza wengine watakwambia kwamba lengo lao ni kuwa tajiri kwa haraka bila kujali njia watakazotumia kupata utajiri huo. Pia kuna wale ambao wanawategemea walezi wao kwa kila kitu. Hawa, hawaoni haja ya kujishughulisha katika kutafuta ajira. Vijana wengine wanachelea kuajiriwa kwa kisingizio kwamba watakosa muda wa kujumuika na wenzao katika shughuli za starehe na anasa. Fikiria pia, kuhusu vijana wanaoshinikizwa na wenzao kukataa ajira. Hawa hulaza damu na kujipiga kifua wakidai kuwa si lazima wafanye kazi.

Kwa mujibu wa Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (2015); Lengo nambari nane linabainisha haja ya kuwepo kwa ajira zenye staha na manufaa kwa wote. Ajira yenye staha ni ile inayoambatana na maarifa na ujuzi alionao mtu. Hata hivyo, ukosefu wa ajira umewafanya vijana kushiriki shughuli zisizokuwa na thamani. Mathalan, wapo vijana waliohitimu katika taaluma mbalimbali ila wanafanya kazi zisizoambatana na maarifa waliyoyapata. Vijana hawa hufanya kazi katika mazingira magumu na yenye kuhatarisha maisha yao. Wengine wanalazimika kufanya kazi kwa muda mrefu na hivyo kuathiri afya yao. Pia kuna vijana wanaopokea malipo duni yasiyoweza kukidhi mahitaji yao ya kimsingi. Ugumu wa maisha huwafanya baadhi ya vijana kuwa wepesi wa kushawishika kushiriki katika matendo maovu na yenye kukiuka maadili ya kijamii ili wafaidike.

Si ajabu kupata baadhi ya vijana wakiwa na malimbikizi ya madeni kotekote. Wao huishi maisha ya kujifichajificha ili kuepuka wadeni wao. Hali hii huwatia fedheha, kuwakosesha uhuru na huwanyima fursa ya kujiendeleza maishani. Kadhalika, ukosefu wa ajira mara nyingi huweza kusababisha mitafaruku katika familia. Huenda wazazi wakakosa kuelewana wao kwa wao au wakakosa kuelewana na wana wao kwa sababu ya kuwa na misimamo tofauti kuhusu suala la ajira kwa watoto wao. Kutokana na hali kwamba vijana wengi hawapati ajira pindi tu wanapokamilisha kozi maalum, kuna uwezekano wa kudidimia na kusahaulika kwa maarifa waliyokuwa wamepata. Mwishowe, vijana wanaojipata katika mazingira ya aina hii huchushwa

na kuchoshwa na makali ya maisha. Hivyo, wanaishia kujitenga na wanajamii ili kuepuka aibu, kusutwa na hata kuelekezewa kidole cha lawama kila mara. Hatima yake ni kushiriki ama katika matumizi ya dawa za kulevya au unywaji wa pombe kupindukia ili kujiliwaza.

Ingawa uhaba wa ajira ni suala linalokumba jamii nyingi, ni muhimu kubaini kuwa zipo njia zinazoweza kutumiwa kukabiliana na hali hii. Vijana wanahitaji kuhamasishwa kuhusu uwezo walio nao katika ujasiriamali ili kuziba pengo la ajira. Aidha wanahitaji kufahamu kuwa si lazima waajiriwe bali wanaweza kujiajiri na hatimaye kuwaajiri vijana wengine. Jambo hili linawezekana iwapo vijana watawezeshwa kwa kupewa nafasi ya kupata mtaji wa kuanzisha au kubuni miradi mbalimbali ya kuwaletea kipato. Vijana wanapopata mitaji hii, wanastahili kupata mafunzo maalum ya namna ya kusimamia miradi hiyo. Vilevile vijana wanaweza kunufaika kutokana na maelekezo watakayopokea kutoka kwa wadau waliobobea katika taaluma maalum. Ni wajibu wa vijana kuungana na kushauriana miongoni mwao ili kujengana. Muhimu zaidi ni kuwa, vijana wana nafasi kubwa katika kuendesha maisha yao; kwani penye nia pana njia.

(a) Fupisha ujumbe wa **aya tatu za kwanza** kwa maneno 90. (alama 8)

**Matayarisho**

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

Teacher.co.ke

**Nakala Safi**

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

(b) Kwa maneno 85, eleza masuala ambayo mwandishi anaibua katika **aya ya nne** na ya **tano**. (alama 7)

**Matayarisho**

Teacher.co.ke

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

**Nakala Safi**

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

Teacher.co.ke

**3. MATUMIZI YA LUGHA** (Alama 40)

(a) Andika irabu zenye sifa zifuatazo: (alama 1)

(i) mbele, juu, tandazwa ..........................................................................................

(ii) nyuma, kati, viringwa ..........................................................................................

(b) Bainisha silabi inayotiwa shadda katika maneno yafuatayo: (alama 1)

(i) bingiria ..........................................................................................

(ii) walimwengu ..........................................................................................

(c) Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo: (alama 2)

(i) anavyojenga

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

(ii) mfariji

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(d) Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Mkulima yupo shambani anapalilia mimea.

..........................................................................................................

(e) Andika sentensi ifuatayo katika umoja: (alama 1)

Waashi walijenga majumba ya kifahari ya kupendeza.

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(f) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo. (alama 1)

Wahandisi walikarabati barabara zote baada ya mafuriko.

(Anza kwa: Barabara ...)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

Teacher.co.ke

(g) Tumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo: (alama 1)

Serikali imebuni mikakati ya kukabiliana na nzige wengi wanaovamia mashamba.

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(h) Alama ya mshazari hutumiwa kutenga nambari. Tunga **sentensi moja** kuonyesha matumizi mengine ya alama ya mshazari. (alama 1)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(i) Kanusha sentensi ifuatayo: (alama 1)

Wanariadha wameenda uwanjani kufanya mazoezi.

..........................................................................................................

(j) Andika sentensi zifuatazo upya kwa kufuata maagizo.

(i) Watalii walifika katika mbuga ya Tsavo walikowaona wanyamapori. (alama 1)
(Tumia 'amba')

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(ii) Mkurugenzi aliwashauri wafanyakazi wajibidiishe kazini. (alama 2)

(Geuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa nomino)

..................................................................................................................................

(k) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Vipepeo wale weupe wanaashiria mvua ya masika inayotarajiwa mwakani.

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(l) Bainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo:

Wanakijiji waliwajengea wakongwe nyumba kwa mawe. (alama 3)

..................................................................................................................................

Teacher.co.ke

(m) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. (alama 2)

Huduma za afya zilipoboreshwa, viwango vya maambukizi vilipungua.

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(n) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 2)

"Watunza mazingira watanadhifisha soko letu kesho." Chifu aliwaambia wafanyabiashara.

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(o) Tunga **sentensi mbili** kuonyesha **matumizi mawili** ya kiambishi **'-ka-'** (alama 2)

..........................................................................................

..........................................................................................

(p) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (alama 2)

(i) bendera ..........................................................................

(ii) ujana ..........................................................................

(q) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (alama 2)

Ngoma hizo zimetengenezwa kwa ngozi laini.

..........................................................................................

(r) Tunga sentensi ukitumia kihisishi kinachoibua hisia za kinyume cha matarajio. (alama 1)

..........................................................................................

(s) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 3)

KN(N + $\bar{S}$) + KT(T) + KN(N + V)

Teacher.co.ke

..........................................................................................

..........................................................................................

(t) Bainisha **maana mbili** zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Jena angalifuata ushauri wa mwelekezi wake angalifaulu.

..........................................................................................

..........................................................................................

(u) Baraste ni kwa barabara, hekima ni kwa .................... na sihi ni kwa .................... (alama 2)

(v) Tunga **sentensi moja** kubainisha **maana mbili** za neno **hema**. (alama 2)

..........................................................................................

(w) Rafiki yako ana mazoea ya kutoa visababu ili asifanye kazi fulani. Andika methali unayoweza kutumia kumwonya dhidi ya tabia hiyo. (alama 1)

..........................................................................................

(Alama 10)

## 4. ISIMUJAMII

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

"Wateja wetu wameagiza bidhaa tena. Katoni mia mbili ziwe tayari kufikia leo jioni. Kazi ianze mara moja!"

(a) Bainisha sajili ya makala haya kwa kutoa mfano kutoka kwenye makala. (alama 2)

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

(b) Fafanua **sifa nyingine nane** za sajili hii ambazo zingejitokeza katika makala haya. (alama 8)

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

Teacher.co.ke

421

0466

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**